

## **Mradi Na. 6226: MRADI WA KUENDELEZA UBUNIFU NA UTENGENEZAJI WA VIFAA VYA TEHAMA**

Katika mwaka wa Fedha 2022/23 **Sh. 3,300,000,000** fedha za ndani zilitengwa kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Kuendeleza Ubunifu na Utengenezaji wa Vifaa vya TEHAMA. Katika Hotuba ya Bajeti ya mwaka wa fedha 2022/23 vipaumbele vilivyoainishwa kwenye mradi huu ni:

- (i) Kujenga Kituo cha Kuendeleza Wataalam, tafiti na ubunifu wa TEHAMA na kufanya maandalizi ya ujenzi wa makao makuu ya Tume ya TEHAMA;
- (ii) Kukiendeleza kituo cha kuendeleza kampuni changa za TEHAMA (ICT startups) cha Dar es Salaam (Soft Centre) na kujenga vituo viwili (2) vya Kanda vya kutengeneza bidhaa za TEHAMA;
- (iii) Kuanzisha Vituo vya Ubunifu na Atamizi TEHAMA katika Wilaya mbili (2) nchini;
- (iv) Kutengeneza mfumo jumuishi utakaouunganisha usajili na uendelezaji wa wataalam na wabunifu TEHAMA nchini (ICT human capital development system); na
- (v) Kuwezesha shughuli za ufuatiliaji na tathmini ya Mradi.

Hadi kufikia **tarehe 31 Disemba, 2022** Wizara ilipokea jumla ya **Sh. 500,000,000** sawa na asilimia **15.2** ya bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Mradi tajwa. Shughuli zilizotekelawa kwa kipindi husika ni kama ifuatavyo: -

- i. Usanifu wa kituo cha ubunifu cha Dar es Salaam umekamilika. Hatua za kusaini mkataba na mkandarasi kwa ajili ya kufanya matengenezo na maboresho ya jengo la TEHAMA ziko katika hatua za ukamilishaji na kituo kinatarajiwa kuanza shughuli zake mwezi Machi 2023.
- ii. Kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa kuainisha mahitaji ya vifaa vitakavyohitajika kwa ajili ya uundwaji wa bidhaa za TEHAMA hapa nchini. Mahitaji yaliyoainishwa yatatumika kuandaa nyaraka za zabuni itakayotangazwa mwezi Machi, 2023.
- iii. Majadiliano na viongozi wa Mikoa ya Arusha, Mwanza na Mbeya ya kupata maeneo ya kuanzisha vituo yanaendelea. Upembuzi na usanifu wa vituo hivyo utafanyika mara baada ya mazungumzo kukamilika mwezi Februari, 2023.
- iv. Mfumo wa usajili wa wataalamu wa TEHAMA umekamilika ambapo wataalamu wa TEHAMA kutoka maeneo mbalimbali wanaweza kujisajili kupitia <https://iprs.ictc.go.tz/>. Aidha, Hatua za ukamilishaji wa maboresho ya mfumo wa usajili wa wabunifu wa TEHAMA unatarajiwa kukamilika mwezi Februari 2023 ambapo utawezesha kuwa na kanzi data ya wabunifu wote wa TEHAMA

(ICT/Digital Innovators) nchini, makampuni ya TEHAMA (ICT Companies), Wawekezaji katika huduma na bidhaa za ubunifu katika TEHAMA (Digital Innovation Investors), Vituo atamizi vya TEHAMA (ICT Incubation Hubs), Vituo vya uendelezaji bunifu za kidijitali (Digital Innovation Accelerators) pamoja na Taasisi za kifedha zinazotoa mitaji kwa wabunifu wa TEHAMA (ICT Innovation Capital Investors).

- v. Wabunifu na Watengeneza bidhaa za TEHAMA 63 wa kanda ya Dar es Salaam walijengewa uelewa wa namna bora ya kukuza bunifu zao ili ziweze kutoa ajira na kuchangia pato la Taifa.
- vi. Miongozo ya taasisi ikiwemo rasimu ya viashiria hatarishi vya miradi na uendeshaji wa shughuli za Tume imeandaliwa. Aidha, mafunzo ya vihatarishi kwa watumishi na wasimamizi wa mradi yatatolewa mwezi Machi, 2023.
- vii. Tume kwa kushirikiana na vyuo vya elimu ya juu vya Dar es Salaam (UDSM), Chuo cha Kilimo Cha Sokoine (SUA), Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA) na Chuo Kikuu cha Ardhi (ARU) imesaini Hati ya Maelewano na Chuo cha Turku (UTU) kilichopo Finland kwa ajili ya kuanzisha Kituo cha *Resilience Academy* hapa nchini. Chuo hiki kitasaidia katika kujenga uwezo na kuongeza ujuzi katika masuala ya TEHAMA hususan sekta ya elimu, tafiti, uendelezaji wa miji, mazingira na uhifadhi wa Data za TEHAMA (*Strengthening digital competences of universities in education, research and service provisioning related to geospatial data, climate risk information management and resilient future development to improve skills and knowledge base of the African Youth for inclusive, safe and resilient urban development*).